Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Tathmini Ya Kipengele Cha Taashira Za Wahusika Katika Tamthilia Ya Kimani Njogu: Mfano Wa *Zilizala*

**Antony Kago Waithiru[1]; Prof. James Ogola Onyango[2]; Prof. Wendo Nabea[3]**

**[1,2,3] Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu**

**Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya**

**Main Author Email: kagoantony3@gmail.com**

**IKISIRI**

Kazi hii inatathmini kipengele cha taashira za wahusika katika tamthilia ya Kimani Njogu. Katika baadhi ya kazi za kifasihi, aghalabu taashira hutumika kama mbinu ya kusana mambo yanayoathiri kitovu cha jamii au yanayoashiria viongozi wa kiimla, wafisadi, wakabila na wenye ubinafsi, na hata uongozi kwa jumla. Kazi hii ni zao la utafiti ulionuia kuchunguza vipengele vya taashira katika tamthilia ya Zilizala. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya baada ya ukoloni na nadharia ya umitindo. Katika tamthilia ya Zilizala ya Kimani Njogu, inadhihirika kuwa mwandishi ametumia wahusika kitaashira ili kuwasilisha fasili tofauti tofauti za dhana moja. Waandishi wa tamthilia za baada ya 2000 wametumia mbinu ya taashira kama njia ya kuwasilisha ujumbe unaohusu uongozi, maadili, siasa na uchumi bila kutaja majina ya wahusika halisi au hata mataifa halisi. Mbinu hii imetumiwa kuwadhihirishia wanajamii mbinu zinazotumiwa na watawala halisi kutawala watawaliwa kupitia vikaragosi vyao, ambavyo ndivyo huchaguliwa na watawaliwa. Aidha, mbinu hii imetumiwa kuashiria jinsi viongozi wengi wanavyothibitiwa na wakoloni kutawala mataifa fukara ya Kiafrika. Matokeo ya utafiti huu yalitarajiwa kuwa na natija kwa wasomi, wahakiki na watafiti wa masuala ya lugha na fasihi kwa kuwa sehemu ya kurejelewa.

**Maneno muhimu**: *taashira, Zilizala, tamthilia, utawala, watawaliwa, vikaragosi*

---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Waithiru, A.K., Ogola, J.O., & Nabea, W. (2020). Tathmini ya kipengele cha taashira za wahusika katika tamthilia ya kimani njogu: mfano wa *zilizala*. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 34-47

---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

## Utangulizi

Wahusika ni viumbe vya kisanaa vinavyoumbwa mahususi na mtambaji ili kuwasilisha dhana fulani. Kwa mujibu wa Wamitila (2010: 369), mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana katika ulimwengu halisi ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu. King'ora (2014) anaeleza kuwa taashira inaweza ikawa kitu au mfano wa kitu kinachowakilisha kitu kingine au kiumbe kisichoonekana kama vile, shetani, mungu na malaika. Hivyo, kulingana naye taashira hupatia kitu, jambo, mtu, hali, hisia au mnyama maana iliyo na uketo au hata ikapanua maana ya kawaida ama ikalipa maana mahususi neno lililoandikwa, ambayo ni tofauti na ile inayoeleweka katika hali ya kawaida na kulifanya liwe ala yenye nguvu katika kuwasilisha ujumbe. Waandishi wa tamthilia za baada ya 2000 wametumia taashira kama leseni ya lugha kuwashilisha ujumbe. Kadhalika, wameweza kuitumia kuficha kasumba. Senkoro (2011) anachambua kwamba wakati mwingine, waandishi wa ubunifu hutumia taashira kuakisi uhusiano kati ya nchi tofauti, uhusiano kati ya wananchi na viongozi, uhusiano baina ya wananchi na mazingira wanamoishi na hata kuakisi mvutano kati ya wema na uovu.

### Udenda

Katika tamthilia ya *Zilizala*, mhusika Meya Udenda amedhihirisha taashira tofauti tofauti. Jina Udenda lilitokana na uhuluti wa utamaduni wa Mzungu na ule wa Mwafrika. Ikumbukwe kwamba, uhuluti ni mojayazo ya mihimili ya nadharia ya baada ya ukoloni. Kwa mfano, Udenda ni taashira ya kiongozi aliyechanganyikiwa na aliyesheheni ubinafsi wa hali ya juu. Kwa mfano, majibizano kati ya Udenda na Angela yanaunga mkono kauli hii. Angela alimuuliza mumewe ikiwa alikuwa na akili timamu na Udenda alimjibu kuwa yu razini, isipokuwa alisadiki kuwa alikuwa amechanganyikiwa tu. Kulingana na Udenda kila mja huwa amechanganyikiwa na hivyo, hakuona kigeni wala kikubwa yeye kuchanganyikiwa (uk. 15).

Meya Udenda ni taashira ya maangamizi na adui wa maendeleo. Hili ladhihirishwa na mama mzee anayeeleza jinsi Meya Udenda alivyosababisha mama mja mzito kuavya mimba. Udenda alikuwa na uwezo wa kuamrisha wamama wapigwe na askari na baada ya askari kutekeleza ile amri, mmoja wao wa wale wamama aliyekuwa mja mzito aliweza kuavya mimba. Kadhalika, Meya Udenda ndiye aliyeamuru mama wafanya biashara wafukuzwe mjini na pia akaamuru vibanda kuteketezwa (uk. 9). Kulingana na Mama katika ukurasa wa 12, Udenda ni taashira ya mwizi. Mama alisema kuwa: "Hebu nikupe siri. Mwizi hujigubika gubigubi lakini baadaye hugunduliwa kwani zake ni arubaini".

Udenda amatumika kama taashira ya mauti. Aliwahamisha wenyeji wa mji wa Rutuba. Yeye mwenyewe alipoiga mtangazaji kwa majinaki alikariri kuwa kwa mujibu wa habari walizozipokea kutoka makao makuu ya mji wa Rutuba, kungekuwa na tetemeko kubwa siku ile. Hivyo, wananchi wote waliombwa wafanye hima kuhama na kuuambaa ule mji bila kusita. Udenda alieleza kuwa yeye kama Meya wa mji ule alikuwa amefanya mipango kabambe ya kuwahamisha wenyeji wa mitaa yote (uk. 16).

Hakika usemi wake Udenda unaweza kuchukuliwa kuwa kweli, lakini ukweli ni kuwa Udenda alinuia kuwabwaga wenyeji wa mji wa Rutuba kwenye Jitochafu. Mauaji ya halaiki si jambo ngeni katika mataifa mengi ya Kiafrika. Kwa mfano, mara nyingi waasi, au hata vikosi vya wanajeshi vya taifa husika huua wananchi wengi kutegemea mrengo vinavyounga mkono au ni vya kabila gani; magaidi wamechangia na pia uongozi huweza kutekeleza mauaji haya kwa lengo la kuwamaliza



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

**ISSN: 2663-9289**

**Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|**
**Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org**
**Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal***

walemavu au kupunguza wapinzani wa serikali tawala. Mfano bora ni aliyoyatenda rais wa pili wa Uganda, Idi Amin Dada. Udenda aliweka hili bayana alipokuwa akizungumza kwa simu huku akibadili na kuchanganya msimbo. Aliuliza ikiwa watu walikuwa wametoka nyumbani na alipojibiwa aliagiza trekta na kila kitu kiwe tayari. Mafundi pia waliagizwa wakae tayari kwa sababu Udenda hangetaka lolote lizuie mipango yake. Trekta ishirini ziliwekwa karibu na Jitochafu na kufichwa karibu na kichaka ili watu wasizione (uk. 6). Lugha aliyochanganya na kubadilisha ya Kiingereza ni taashira ya ukoloni mamboleo. Trekta nalo laashiria maangamizi ya Waafrika ili viongozi wanyakue maeneo yanayoachwa mahame. Jitochafu ni taashira ya kaburi la halaiki.

Udenda ni taashira ya kiongozi anayetumia mbinu za kigeni kutawala wananchi wa mji wa Rutuba, na hivyo kukuza na kuendeleza ukoloni mamboleo. Atetea mbinu zake za kuendeleza udhalimu dhidi ya mkewe Angela kwa kusema kuwa: "kuna mambo ambayo una haki nayo na mengine usiyokuwa na haki nayo. Na hilo ulilolifanya leo, kujaribu kudadisi maisha yangu, huna haki nalo" (uk. 17). Hili ladhihirisha kuwa, Udenda ni taashira ya kiongozi asiye na uzalendo. Kiongozi asiyejali kizazi cha kesho, anayekuza na kupalilia uhanithi wa taifa, kwa mfano, mji wa Rutuba, ambao ni taashira ya taifa la Kiafrika. Badala ya kupalilia jamii na viongozi wa kesho – vijana – anawaangamiza polepole.

Hili lawekwa bayana na Udenda anapomuuliza mkewe kuwa, nani aliyemfahamisha Inspekta Chatu kuhusu shughuli zake na wenzake walipoleta dawa za kulevya nchini na kuzisambaza mashuleni na mitaani (uk. 18). Vijana ni taashira ya viongozi wa kesho. Ndiposa Udenda na viongozi wengine dhalimu wanajaribu kuwaangamiza kwa kusambaza dawa za kulevya katika mashule na mitaani. Kadhalika, kupitia vitendo dhoofu vya Udenda, ilibainika kwamba Inspekta Chatu ni taashira ya mfanyikazi wa umma aliyewajibika na mzalendo. Alionekana kufanya juu chini kudidimiza juhudi za Meya Udenda za kuwaangamiza vijana (uk. 18). Msafara wa wanawake aliokuwa nao Udenda ni taashira ya mataifa mengi ya Ulaya yanayonyonya bara la Afrika madini, fedha na hata wafanyakazi wenye stadi mbalimbali. Mataifa haya ndiyo huingilia uongozi wa mataifa ya Kiafrika. Hata hivyo, utamaduni wa Kiafrika unachangia ukoloni mamboleo kutokana na mila na desturi zilizopitwa na wakati. Kwa mfano, Udenda anashikilia kauli kuwa mwacha mila ni mtumwa, kuashiria kwamba baadhi ya vipengele vya utamaduni wa Kiafrika ni taashira za minyororo ya utumwa kwa Waafrika. Alipokanywa na mkewe dhidi ya kupunguza msafara wa wanawake, alijitetea kwa kusema kuwa siye aliyewatafuta ila ni wao wenyewe waliomfuata. Udenda alisisitiza kuwa wanawake ndio waliomwandama na kwa mujibu wa utamaduni wa Kiafrika, ulimruhusu Udenda kufuatwa au hata kuoa wanawake wengi awezavyo. Alimkumbusha Angela kuwa mwacha mila ni mtumwa na hivyo, yeye aliifuata tu unyounyo. Lakini akumbuka kuwa wale mabenati wanapenda umaarufu na uwezo wake ila siye wanayempenda kwa mapenzi ya dhati kama vile Angela alivyompenda (uk. 22).

Aidha, Udenda ni taashira ya viongozi wasiowajibika. Udenda alipokuwa Diwani wa mji wa Kusudi alikuwa anakaa na familia yake – mkewe na watoto – pamoja na wafanyakazi kama vile Diana. Lakini alipochaguliwa kama Meya wa mji wa Rutuba aliambaa kwake pamoja na familia yake kwa muda usiopungua miaka mitatu. Angela alilalamika kuhusu uadimikaji wa bwanake nyumbani na kuhusu upungufu wa mahaba ya Udenda kwake na watoto wao. Analalamika kuwa angetaka Udenda arejee nyumbani ili atekeleze wajibu wake kama mzazi. Takriban miaka mitatu wanawe Udenda walikuwa wanamsikia redioni akionya raia. Angela alilalama kuwa alikuwa amechoka kulea watoto peke yake ilhali Udenda



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

alizunguka mitaani. Alichelea kumuomba arudi nyumbani hata kama wangeishi mbalimbali kudhihirisha upweke alokuwa nao Angela (uk. 24). Udenda alichangia mhimili wa nadharia ya baada ya ukoloni ya uasi. Tamaa ya ukoloni mkongwe ilimlazimu Diwani Udenda kuacha familia yake. Tamaa ya mali ilimfanya ajitenge na marafiki na jamaa.

Zaidi, Udenda aashiria viongozi ambao husaliti wananchi waliomchagua pamoja na taifa lao kwa jumla badala ya kuwahudumia. Udenda alisaliti wananchi waliomchagua na kuwaangamiza. Kadhalika aliwasaliti na kuwaambaa wana wake pamoja na mkewe kwa zaidi ya miaka mitatu akiwa uongozini. Mathalani, Udenda ni taashira ya Magavana, Wabunge, Wawakilishi wa Wadi, na wengine wengi nchini Kenya kwa mfano, ambao husaliti Wakenya kila uchao. Badala ya kuwahudumia wananchi, wao hunyakua mali ya umma na kujinufaisha wao wenyewe na familia zao.

Hata hivyo, Udenda pia ni taashira ya mpiganiaji haki za wananchi. Kumba adhihirisha hili anapomkumbusha Udenda kuhusu mienendo yake kabla ya kuwa mumunye na kuharibikia ukubwani. Alimkumbusha Udenda kuwa alikuwa mchezaji, mrari wa umma na mtetezi wa haki za wananchi. Hivyo ndivyo Kumba alimkumbuka Udenda. Udenda alipokuwa chuo kikuu aliongoza migomo kupinga utawala wa dhuluma nchini mwao na kwingineko. Alikuwa na msimamo uliopinga Amerika. Kutokana na ukakamavu wake, ujasiri na upiganiaji wa haki, Angela alivutiwa naye sana. Hivyo, aliweza kuteka nyoyo za wengi akiwemo Angela. Udenda aliienda Nikaragua na Mashariki ya Kati akitetea haki za binadamu na kuhubiri umoja, haki na usawa (uk. 32).

Bara la Amerika ni mojawapo ya mataifa tajiri na yenye zana za kivita za hali ya juu, kando na uwezo wake wa kupigana na maradhi mbalimbali, njaa, ufukara na ufisadi. Ni taifa ambalo husifika kwa fursa nyingi za kujiendeleza kiuchumi na Waafrika wengi na la uhuru na demokrasia iliyokomaa. Ni taifa ambalo liliwahi kutawaliwa na Waingereza kabla ya kupata uhuru. Kiuyakinifu, Kimani Njogu alitumia neno Amerika kama taashira ya mataifa yaliyojiweza kiuchumi ya Ulaya. Mataifa haya hunyonya ya Afrika kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa upande mwingine, Nikaragua na Mashariki ya Kati ni taashira za mataifa ya Asia yaliyojiweza kiuchumi, ambayo husaidia mataifa masikini ya Kiafrika kupiga hatua kimaendeleo. Mathalani, Uchina, Bara Hindi, Israeli na mengine mengi.

Maelezo ya Kumba kwa Udenda yaashiria hali halisi ilivyo katika mataifa mengi masikini ya Kiafrika. Viongozi wengi Waafrika walianza kujitosa katika dimbwi la siasa wakiwa wanafunzi vyuoni. Mle walikuwa wapiganiaji wa haki za wanafunzi. Kwa misingi hiyo, wao walikuwa taashira za viongozi ilhali wanafunzi walikuwa taashira za wananchi. Vyuoni wao huanza wakiwa watetezi wa haki za wanafunzi na hupata sifa hata miongoni mwa wanasiasa. Wapatapo makini ya wanasiasa, tembo hutiwa maji na mwema huwa mui bila hata ilani. Kwa misingi hii, ngozi ya chui ni taashira ya tamaa na ubinafsi. Kumba alilalamika kuwa Udenda alibadilika punde tu alipovaa ngozi ya chui na akakakosa kujulikana wala kutambulika tena (uk. 36).

Kadhalika, Udenda ni taashira ya viongozi wasaliti. Alisaliti wananchi na kuwalaghai. Kumba alidhihirisha hili alipoeleza kwa masikitiko huku akitizama hadhira kuwa, Udenda alikuwa amebadilika kweli. Udenda waliyemjua mle chuoni alibadilikia ukubwani na kuwa mumunye. Haki za umma hakuzijali tena, ila chake ndicho alichojali. Ubinafsi ulimvaa tangia unyayo hadi utosini. Haki za raia alibatilisha huku wakimwita mja wa umma (uk. 40 – 1). Hivyo basi, Udenda ni taashira ya viongozi Waafrika ambao ulafi, ufisadi, ukabila na ubaguzi ndizo nguzo zao maishani. Kuna wahusika wengine ambao wamechangia pakubwa katika ujenzi wa mhusika Udenda kitaashira.



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Mwandishi alifanikisha hili kupitia, ujenzi wa wahusika waliomjenga au kumbomoa mhusika Udenda. Mzee Teleza kwa mfano, ni taashira ya Waafrika wazalendo wanaonyanyaswa na viongozi kama Udenda. Ni Mja mwenye utu na anayejali wengine. Kumba alieleza kuwa mzee Teleza angeweza kusikitishwa na kifo cha Kumba tofauti na rafikiye Udenda ambaye hana utu, alibadilika sana akilinganishwa na yule Udenda waliyemjua chuoni (uk. 42). Mwandishi wa mchezo wa Puma na Memetuka – Mwalimu Sega – ni taashira ya wasanii Waafrika wanaotumia fasihi kama ala ya kubadili uongozi na utawala dhalimu barani Afrika, kama ule wa Diwani Udenda.

Zaidi ya hayo, mwandishi alitumia wahusika wanawake kuzalisha taashira za mhusika Udenda. Taashira hizi zinaashiria ukakamavu wa waandishi Waafrika na uzalendo wao unaowafanya kutumia taashira za wahusika wadogo kukuza taashira za wahusika wakuu, kwa minajili ya kukemea uongozi mbaya. Mathalani, Hekima Amara ni mhusika aliyetumiwa na mwandishi kukuza taashira zinazoanika peupe viongozi dhalimu wa Kiafrika kitaashira, kama Diwani Udenda. Hekima Amara ni taashira ya wanawake Waafrika wapiganiaji haki za wananchi. Ni mwanamke jasiri na mwenye kujitolea kutetea mali ya umma. Aliyedhubutu kupigania ardhi ya umma isinyakuliwe na Diwani Udenda. Mama huyu alimpa kiwewe Diwani Udenda. Hili lilidhihirishwa naye Diwani alipoomba msaada wake Bwana Inspekta na kumweleza kuwa kuna mama aliyekuwa akimzuia kujenga ploti yake. Ploti aliyotunukiwa na madiwani wenzake. Diwani Udenda alieleza kuwa Hekima Amara alikuwa amemghadhabisha kiasi kwamba hakutaka kuisikia sauti yake. Kwa mujibu wa Hekima Amara, kiwanja kile alichokuwa akitaka kujenga Diwani Udenda kilikuwa cha shule na aliwahamasisha wazazi na wanafunzi kukipigania kiwanja chao. Jambo hilo lilimkasirisha Diwani Udenda na ndiposa akamuomba Bwana Inspekta akitumie *crown* kumkomesha na kumnyamazisha Hekima Amara (uk. 57).

Aidha, huu ni unyamazishaji wa wazalendo wanaojaribu kupigania haki za wananchi. Unyamazishaji ni mojawapo ya mihimili mikuu ya nadharia ya baada ya ukoloni. Kadhalika, Diwani Udenda ni taashira ya uongozi uliosheheni ufisadi, uvunjaji wa sheria, ubinafsi na ukiukaji wa haki za kibinadamu. Hakika ni uongozi unaotoa uvundo wa hali ya juu. Diwani Udenda anathibitisha hili anapodondokwa na maneno ya kukirihisha na kusema kuwa: Sheria ni nini? Twaibatilisha kila siku! Nani anayejali siku hizi? Kila mwamba ngozi anavuta kwake. Na hakuna kuku anayemdonolea mwenziwe (uk. 58). Usemi wake Diwani Udenda wadhihirisha ubinafsi uliokidhiri baina ya viongozi wengi katika mataifa mengi barani Afrika, ikizingatiwa kwamba Diwani Udenda ni taashira ya viongozi dhalimu barani Afrika.

Zaidi ya hayo, Meya Udenda ni taashira ya kiongozi Mwafrika, ambaye hunajisi na kuwadhulumu wanawake. Atieno alisema kuwa Udenda alimharibia maisha na kumchafua. Mama anamliwaza ingawa yeye pia anakasirishwa na vitendo vya Udenda vya unyama. Pia Udenda ni taashira ya kiongozi mnafiki. Aliwagandamiza wananchi baada ya kuwalaghai kuwa kila kitu kitakuwa shwari. Baada ya kuwaahidi maeneo yasiyo na mitetemeko aliwaangamiza na kutupa maiti zao kwenye Jitochafu.

Hususani wanawake wa Kiafrika hudanganywa na hatimaye hunajisiwa; kisiasa, kimwili, kihisia, kiuchumi na kidini. Kwa mfano, Atieno analalamika kuwa: "*(Anaanza kutulia sasa.)* Udenda aliponiletea zawadi mara ya kwanza, niliipuuza. Nikafikiri ni ukarimu wake; ni wema na huruma zake. Mapenzi ya mwajiri wangu juu ya kazi



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ninayofanya" (uk. 69). Kama ilivyotajwa katika sura hii, Atieno ni taashira ya mwanamke Mwafrika, ambao hunaswa na mitego ya viongozi Waafrika. Uhusiano kati yake na mwajiri wake Udenda ni taashira ya uhusiano kati ya wananchi Waafrika na viongozi wao. Atieno alinajisiwa kimwili alipokuwa amelala chumbani mwake, kuashiria unajisi unaotekelezwa na viongozi Waafrika dhidi ya mataifa wanayoyaongoza.

Hakika Udenda ni taashira ya mnyama hayawani. Mama kwa ghadhabu alisema kuwa: *(Kwa hasira nyingi.)* Mnyama! Hayawani! Kichaa! Wazimu! (uk. 70). Pia ni taashira ya Mbeberu. Alitumia mali aliyoyanyakua, uwezo na cheo chake kuwadhulumu wananchi. Watawaliwa wasadiki hili kupitia Mama anayesema kuwa: Sauti yake ina nguvu na mwangwi kuliko yako. Anajulikana mahakamani (uk. 74). Hivyo basi, Atieno, aliyebakwa na kukosewa heshima hasikizwi wala kupewa haki mahakamani, ilhali Udenda asiyeheshimu maisha ya binadamu na uhai wake anadhibiti kila kitu mahakamani. Hili laashiria kiwango kile haki, usawa na ukweli zimenajisiwa katika mataifa mengi ya Kiafrika.

Udenda pia ni taashira ya wabunge katika mataifa mengi masikini ya Kiafrika. Wabunge katika mataifa mengi barani Afrika hubatilisha sheria ili kujilinda na kujinufaisha. Ubinafsi wao uliokithiri huwaongoza kwa utaratibu katika kujipatia nyongeza nono za mishahara na marupurupu si haba bila kujali wananchi wanaoangamizwa na janga la njaa, maradhi, dawa za kulevya, pombe haramu, hali mbaya ya usalama pamoja na changamoto za maisha kwa jumla zinazochangiwa na ukosefu wa maendeleo endelevu. Mama anasawiri uhalisi huu anaponasihi Atieno apunguze hasira. Alimfahamisha kuwa, hata kama yaliyomkumba hakika yalikuwa makubwa yasiwakatishe tamaa ila yawe funzo kwao. Udenda alimnajisi Atieno kwa sababu alikuwa na uwezo na hata kumshitaki ingekuwa bure kwa sababu alikuwa na uwezo wa kubatilisha sheria ili kujilinda yeye binafsi (uk. 74).

Udenda analaghai watu na hata kujitapa kuwa ana sauti ya kuteuka, ukweli na haki. Sauti ya kuteuka kama anavyoeleza Udenda ni taashira ya vyombo vya habari barani Afrika, ambavyo huwa visiki katika shughuli za kupata uhuru. Ni vyumba vya babari ambavyo hutumiwa na viongozi Waafrika kutoa ujumbe wa kupotosha wananchi. Kadhalika, ni vyumba ambavyo hutumia vyombo vyao kupigia upatu vikaragosi vya ukoloni mamboleo katika mataifa maskini ya Afrika. Aidha viongozi Waafrika huvitumia vyumba hivi vya habari kama visesere vyao vya kueneza uvumi. Kwa mfano, Udenda anawakumbusha wakazi wa Sikitiko ripoti iliyokuwa imepeperushwa kutoka redioni. Kupitia ripoti ile sauti ya kuteuka kama anavyoitaja Udenda ilitamkwa bila kelele. Udenda aliwakumbusha wenyeji wa mtaa wa Sikitiko kuwa baada ya muda mfupi kungekuwa na zilizala katika mtaa wa Sikitiko. Aliwaonya dhidi ya madhara ya zilizala ambalo lingewameza wote kama hawangeabiri 'Matatu' ya Kifaduro. Aliwahimiza wajipurukushe kabla ya utumbo wa ardhi kuanza kucheza na kusababisha zilizala, mtutumo, mtikisiko au mtetemo (uk. 83).

Udenda ni taashira ya muuaji. Ndiposa Kumba alimwita chui huku yeye akijiita mbuzi. Chui ni mnyama mlanyama ambaye anafanana na paka mkubwa na mwenye kasi sana na hupatikana katika janibu za Asia na Afrika. Katika matumizi yake ya kawaida neno hili likihusishwa na mwanadamu, humaanisha mja mwenye ukali mwingi hasa wenye kudhalilisha—yaani mtu mla watu. Mbuzi kwa upande mwingine ni mnyama mlanyasi, afugwaye anayefanana na swara. Mwituni na mbugani, wakati mwingi mnyama chui hula swara sana sana. Ikizingatiwa kwamba swara na mbuzi wanafanana, chui huweza kumla mbuzi pia amuonapo na apatapo nafasi. Hivyo


© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

basi, uhusiano kati ya chui na mbuzi ni wa maonevu, manyanyaso, mateso na hatimaye mauaji. Kwa upande mwingine, uhusiano kati ya binadamu na mbuzi huwa wa kufaana na hatimaye mbuzi hufanywa kitoweo. Kipanga ni ndege mkubwa anayepaa juu sana angani na ambaye hula vifaranga wa kuku. Kiuyakinifu, chui na kipanga ni wanyama ambao huishi kutokana na kuangamiza wengine kama vile mbuzi na vifaranga. Kwa misingi hii, chui na kipanga ni taashira za viongozi Waafrika wauaji kama Udenda – ilhali mbuzi, kuku na vifaranga ni taashira za wananchi Waafrika kama Kumba. Mintarafu ya haya, Kumba alishangaa na kujiuliza kama kungetokea siku ambapo chui na mbuzi wangekuwa marafiki au hata kipanga angemlelea kuku vifaranga wake (uk. 87). Hakika ikizingatiwa kwamba chui humla mbuzi na kipanga humla kifaranga, siku aliyoishangaa Kumba kukucha ingeishi kuwa giza totoro lisilokucha hata kwenye ndoto.

**Mama**

Mama ni taashira ya nchi ambazo hutunza wenyeji wake. Wakati Udenda anadhihirisha kutojali na kuwadharau watu anapowarai waingie Matatu ya Kifaduro, Mama alidhirisha upendo utu na heshima. Udenda hajali wazee na wasiojiweza. Alihimiza mwenye nguvu apishwe ilhali asiye na nguvu akanyangwe na mwenye nguvu. Pia ni taashira ya mwananchi anayejali taifa lake na wenzake. Mama aliwaombea wajukuu wake na taifa lake kwa jumla. Wakati Udenda alimwonyesha Mama madharau na unyama, yeye alimjibu kwa heshima, utu na upendo. Udenda anamwimbia Mama na kumfahamisha kuwa kila mtu angeuchukua mzigo wake mwenyewe. Kwamba kila mtu angejibebea gogo alilojitwika mwenyewe na kisha akaangua kicheko (uk. 8). Kitendo cha Mama cha kuwaombea wananchi wenzake pamoja na taifa lake chamwashiria kama taashira ya mzalendo anayejali wenzake.

**Nari**

Nari ni taashira ya mabadiliko. Aliwahamasisha na kuwazindua Wote ambao ni taashira ya wananchi. Nari na Wote ni wahusika katika tamthilia ya *Zilizala*. Kwa mfano, katika mazungumzo kati ya Nari na Wote, Wote wanasema kuwa walikuwa wanaona kila kitu. Nari anawatia chonjo na kuwahamasisha kuwa zaidi ya kujua kila kitu, walikuwa na dhamira ya kurekebisha mambo. Nari aliwazindua Wote na kuwapa motisha (uk. 78). Nari pia ni taashira ya mwanamapinduzi. Aliwahamasisha wananchi kutia bidii katika harakati za mapinduzi alipowahimiza wawe wabunifu. Hii ni kwa sababu, mahala alipowakumbusha kuhusu, Barabara ya Shango ni taashira ya eneo la ubunifu na uvumbuzi. Aliwapa changamoto alipowauliza kuwa: "*(Akitazama hadhira.)* Barabara ya Shango; nafasi ya wasanii, nafasi ya ubunifu. Nafasi yangu, yako, yake, yetu. Je, unaitumia vipi?" (uk. 53). Nari anaendeleza mhimili mmojawapo wa nadharia ya baada ya ukoloni, mhimili wa uzinduzi.

Nari anahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa elimu katika harakati za mapinduzi. Kusoma kama Nari anavyosema ni taashira ya ala muhimu inayotumiwa na Waafrika wazalendo katika mataifa mengi fukara ya Kiafrika kupigana na ukoloni mamboleo. Ndiposa Nari anasisitiza umuhimu wa kuendeleza vita dhidi ya ukoloni mamboleo. Hili alidhihirisha alipoeleza kuwa ingewalazimu kusoma na kujifunza kutokana na miji ile mingine. Nari aliwasisitizia umuhimu wa kujitathmini na kujiuliza kile kilichowawezesha watu wa Tegemeo kuusafisha mji wao. Aliwaasa wasome na watafakari kuhusu kile kilichowawezesha; watu wa Wema, watu wa Rehema na watu wa Shibe kuupiga msasa mji wao (uk. 79).

**Mtambaji**

Mtambaji ni taashira ya tumaini duniani kwa watu. Ndiposa spotilaiti inamwangazia yeye pekee. Katika



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kianzio (uk. 2 – 4), Mtambaji amegusia wahusika wengine mbalimbali wanaodhihirisha kuwa yeye ni taashira ya matumaini duniani kama vile Nari na wasanii, hususani katika mataifa ya Kiafrika. Hadhira anayozungumza nayo ni taashira ya wananchi wazalendo wanaopenda amani, haki na ukweli. Hili ladhihirishwa na uwezo wa nafsi ya Mtambaji wa kumsuta. Wahusika hawa ni pamoja na; Wale, ambao ni taashira ya mabwanyenye waliosheheni ubinafsi, ulafi na ufisadi. Nabii ambaye ni taashira ya mzalendo aliyeelimika, ilhali ndoto yake ni taashira ya elimu ambayo husaidia watu kuona mbele. Kwa misingi hiyo hiyo, Mnyama hatari wa baharini ni taashira ya Mbeberu. Naye Dereva Kombo ni taashira ya viongozi wa vyama vya kisiasa ambao hupotosha wafuasi kwa kuwalaghai.

**Atieno**

Atieno ni taashira ya wananchi wazalendo. Yeye ni taashira ya suluhu ila si tatizo kama Pakistindi katika mataifa ya Kiafrika. Ndiposa anaangazia kinachosababisha mitetemeko na radi za mara kwa mara barani Afrika (uk. 12). Atieno na Mama ni taashira ya wanawake Waafrika katika mataifa mengi ya Kiafrika. Wanawake Waafrika hunyanyaswa na kudunishwa, hasa katika masuala ya uongozi. Katika onyesho la tatu, kitendo cha pili chatangulizwa na maelezo yanayoashiria taswira halisi katika mataifa mengi barani Afrika. Barani Afrika, mwanamke husukumwa mbali na uongozi na hutengwa katika uamuzi wa masuala muhimu yanayoathiri uongozi wa taifa husika. Wao huchukuliwa kama viumbe duni. Ndiposa katika maelezo yale, Atieno na Mama wanaonekana mbele kabisa jukwaani kuashiria mabadiliko.

Halikadhalika, wanawake Waafrika wanakumbana na dhiki chungu nzima. Hili laashiriwa na hali ya Atieno. Pale jukwaani, Atieno analia kwa uchungu na Mama anajaribu kumtuliza. Ikizingatiwa kwamba uchungu alionao unaomliza ulisababishwa na Udenda aliyemnajisi, basi hii ni ishara tosha kuwa viongozi wa Kiafrika ndio chanzo cha matatizo yanayowavamia wanawake Waafrika. Kwa mfano, maelezo yanayoeleza onyesho linapoanza yanadhihirisha kuwa wanawake wameanza kuwa suluhu kwa matatizo yanayolikumba bara la Afrika kwa jumla. Mwandishi amesawiri Atieno na Mama wakiwa mbele kabisa jukwaani. Ingawa Atieno analia kwa uchungu, sehemu waliyochukua jukwaani yaashiria bayana kuwa wanawake Waafrika hawajakata tamaa katika harakati za kupigania uhuru wa Mwafrika kutoka kwenye minyororo ya ufukara (uk. 68).

**Angela**

Angela ni jina la kigeni linalotokana na neno 'Angel' la Kiingereza. Hivyo, lenyewe laashiria utamaduni mgeni barani Afrika. Jina Angela lilitokana na uhuluti wa utamaduni wa Mzungu na ule wa Mwafrika. Uhuluti ni mojayazo ya mihimili ya nadharia ya baada ya ukoloni. Ni mhusika anayechangia pakubwa katika mapinduzi na mabadiliko ya uongozi. Ndiposa mwandishi anamsana kama mwanamapinduzi. Angela anapinga itikadi na imani za utamaduni wa Mwafrika uliopitwa na wakati, ambapo mwanamke hana nafasi ya kutoa maoni na hisia zake wala uamuzi. Angela ni mkewe Udenda wa Panuka na ni mzazi. Angela ni taashira ya mkombozi. Anapigania haki za binadamu, hususani watoto na vijana.

Kwa mfano, Angela alipoulizwa na mumewe Udenda kama ni yeye aliyetia sahihi ili misitu isiuzwe, alimjibu kuwa: "Ndiyo … *(Anakaribia na kutazama hadhira.)* Ningefanya nini? Mume wangu amechukulia kwamba ulimwengu ni wake auhodhi. Ameuza kila kitu: makaburi … barabara … misitu. …" (uk. 28). Hili laashiria Waafrika wachache wazalendo ambao hutunza mazingira. Mathalani, baadhi ya wahusika kama vile; Angela, Nari, Kumba na wendawazimu wa Bewa la Pevu kama wanavyorejelewa na Udenda ni taashira za wapiganiaji



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

haki za wanyonge. Udenda analalamikia mkewe kuwa ameanza kumea pembe. Angela asemekana na mumewe kuwa alikuwa na pembe ndefu kama za faru. Ikizingatiwa kwamba kifaru ni mnyama mwenye nguvu na ujasiri mwingi, ni kuashiria kuwa Udenda alimwona Angela kama tisho kwa uongozi wake dhalimu. Alimjongelea na kumzunguka huku akimtazama kichwani. Alimkumbusha Angela kuwa hapo zama alikuwa mtiifu na alipoambiwa anyamaze alinyamaza. Utiifu wake ulimpendeza Udenda ambaye kila alipomwambia afanye jambo alifanya bila ubishi. Kila alipoambiwa abweke alibweka. Lakini tangu Angela aanze kushirikiana na akina Nari, Kumba na wendawazimu wa Bewa la Pevu, alianza kumpinga Udenda. Udenda hakupendezwa na mabadiliko hayo yaliyompelekea mkewe kupandwa na shetani, akawa zumbukuu asiyejua tena kuja matao ya chini kama mkewe ila alipandisha tu. Lililomuudhi Udenda sana ni kile kitendo cha Angela cha kuyachunguza mambo yake na kutia sahihi kupinga uharibifu wa misitu. Kile Udenda alisahau ni kuwa misitu ilikuwa mali ya umma (uk. 19 – 30).

Angela ni taashira ya bara la Afrika. Ndiposa jinsi bara la Afrika linavyosalitiwa na viongozi Waafrika, Angela pia anasalitiwa na mumewe Udenda. Udenda alioa mwanamke Mwitaliano na wakapata watoto pamoja (uk. 70). Alimsahau Angela na kumwachia majukumu yote ya nyumbani punde tu alipomwoa Mwitaliano. Alichoachiwa Angela cha kujivunia ni jina tu – *The Mayor's wife* (uk. 31). Mwili wake Angela ni taashira ya mataifa mengi barani Afrika. Mataifa haya hunyonywa na viongozi na mazingira huharibiwa ovyo. Hili liliashiriwa na vipigo na matusi ya Udenda kwa mkewe Angela. Udenda alipomuahidi kumcharaza, Angela alijibu kwa dharau kuwa hata angemcharaza haingekuwa mara yake ya kwanza kucharazwa na Udenda. Angela alimrejelea mumewe kama Meya mtukuka-mpandisha-mlingoti. Angela alimuonya Udenda kuwa, ingawa angempiga kama alivyozoea, siku itafika na manyanyaso yatafikia tamati kuashiria matumaini ya siku ambayo bara la Afrika litajikomboa kutoka kwenye minyororo ya ukoloni mamboleo na ulofa (uk. 28).

**Makundi**

Kikundi cha "Mjumuishi" ni taashira ya chama cha kisiasa cha mapinduzi katika mataifa maskini ya Kiafrika. Kikundi hiki kilipata jina hili kutokana na kitenzi kujumuisha. Kujumuisha ni kufanya watu wachanganyike pamoja, au washiriki kwenye shughuli inayofanywa na wengine. Viongozi wa Kiafrika hupigishwa mshipa na umoja wa wananchi na pia uwezekano wa wao kufahamu haki zao. Majibizano kati ya Udenda na mkewe yalithibitisha hili. Udenda kwa ukali zaidi alimjuza Angela kuwa nduru za kuaminika zinasema kuwa amejiunga na kikundi cha "Mjumuishi". Udenda alimuuliza yeye na wanakikundi wenzake wanakutana kujumuisha na kupatanisha akina nani? Angela bila woga alimjibu kuwa wa kulaumiwa ni Mwenyezi Mungu aliyempa macho, masikio na ulimi (uk. 21).

Mafundi wanaorejelewa na Udenda (uk 32) ni taashira za wauaji ambao huua watu kabla ya kuwatupa kwenye Jitochafu. Hii ni mojawapo ya changamoto zinazokumba mataifa ya Kiafrika. Viongozi wengi Waafrika hawana heshima kwa maisha ya binadamu. 'Mafukara wa Ulimwengu' wa mji wa Kusudi ni taashira ya wananchi fukara katika mataifa fukara ya Kiafrika. Kadhalika, Kikundi cha Ujumuishi ni taashira ya wakombozi. Hawa ndio wakombozi wanaojinyima na hata kuhatarisha maisha yao kupigania ukombozi wa Waafrika. Masomo wanayopata wanakikundi hiki kutoka vitabuni ni taashira ya silaha ya kupigania uhuru wa Mwafrika. Katika ukurasa wa 68, mwandishi amemsawiri Kumba akiwaongoza wenzake wa Kikundi cha Ujumuishi katika mazungumzo makali. Wana vitabu wanavyosoma huku wengine wakiandika. Wengine wao wanatunga nyimbo ilhali



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

wengine washiriki mazungumzo ya ishara. Wanapoendelea na yale mazungumzo wanabishana na pia wanasikilizana. Hata hivyo, mwandishi atufahamisha kuwa sauti zao hazisikiki mpaka hapo baadaye (uk. 68). Maelezo ya mwandishi yanalandana na maoni ya mtafiti.

Kikundi cha Haki za Wanawake Afrika (HAWAA) ni taashira ya wakombozi. Kimsingi, neno 'hawaa' hutokana na mwanamke wa kwanza kuumbwa duniani katika shamba edeni (United Bible Societies, 2004). Hata hivyo, katika lugha ya Kiswahili, neno hili hurejelea hamu ya kutaka kufanya mapenzi; yaani nyege au ashiki. Lakini kikundi cha HAWAA kinaashiria wanawake Waafrika wenye hamu ya kulikomboa bara la Afrika. Tofauti na vita vya uhuru kutoka kwa Mbeberu vilivyohusisha ala kama; bunduki, panga, visu, vilipuzi aina tofauti tofauti na nyinginezo nyingi; vya kumng'oa mkoloni Mwafrika vinahusisha; elimu, kampeni na umoja ulio na lengo maalumu – uhuru. Kadhalika vita dhidi ya Mzungu vilihusisha MAU MAU lakini vita dhidi ya Mzungu mweusi vinahusisha wanawake Waafrika. Wanawake hawa wamekuwa katikati mwa miji lakini sasa kwa mujibu wa Njogu wameanza kutokeza vitongojini (uk. 74).

Bewa ni eneo lililo na viwanja na majengo ya Chuo Kikuu. Pia huitwa ndaki. Pevu ni neno linalorejelea jambo au kitu kilichokomaa au kilichopevuka au kilichoiva. Hivyo, maneno haya yanapoletwa pamoja na kuunda Bewa la Pevu, ni kumaanisha kuwa yanarejelea eneo lililo na viwanja na majengo ya Chuo Kikuu linalosheheni vijana walioiva au waliokomaa kiakademia. Ukomavu huu ndio unaowapelekea kujihusisha na maswala ya uongozi na utawala. Tofauti na wananchi wengine, wao wamekomaa kimawazo, kifalsafa, kiitikadi na kiimani na hivyo wanaweza kuona 'mbele' na kupata ruwaza ya taifa lao miaka kadhaa ijayo. Bewa la Pevu lenyewe ni taashira ya baadhi ya Vyuo Vikuu vinavyochangia maendeleo endelevu katika mataifa fukara barani Afrika.

Katika misingi hii, mintarafu ya madhumuni ya kwanza, ilibainika katika utafiti huu kuwa vijana wa Bewa la Pevu ni taashira ya Waafrika wazalendo, ambao ndio watakaolikomboa bara la Afrika kutoka kwenye minyororo ya uongozi mbaya, ufukara, dhuluma, ufisadi na usaliti. Vijana hawa wanaashiria Waafrika wazalendo, shupavu na wakakamavu ambao hutumia vifaa vya kiteknolojia na utandawazi kukabiliana na umasikini – zilizala – uliokita mizizi katika mataifa mengi barani Afrika. Mbinu muhimu wanayotumia ni kuelimisha na kufahamisha Waafrika wengine wengi wasioelimika kuhusu chanzo cha ulofa, dhuluma, uongozi na utawala mbaya, dhiki na matatizo – *zilizala* – yanayolikumba bara la Afrika kwa jumla. Baadhi ya vifaa wanavyovitumia ni mtambo wa tarakilishi ambao ni taashira ya utandawazi barani Afrika. Nari anaeleza kuhusu dhuluma walizozipata kutoka kwake Udenda na anamkumbusha Atieno kuwa Udenda alihakikisha kuwa walitiwa korokoroni bila hatia. Udenda alibomoa matumaini ya vijana. Nari anasema kuwa vijana wa Bewa la Pevu wamechoka na hivyo, wanazuru kila janibu kuoyesha chimbuko la zilizala huku wakiongozwa na dadake Atieno. Nari akiri kuwa vijana hawa wamegundua kwa kutumia mtambo wa tarakilishi chanzo cha ulofa na dhuluma zinazowakumba kila uchao. Alalamika kuwa hakika wamechoka (uk. 79).

Jina Poromokeni linatokana na kitenzi poromoka, ambacho humaanisha kuanguka na kusambaratika au kutawanyika kwa mfululizo. Hivyo, Kundi la Poromokeni lilipata jina hili kutokana na msukumo wao wenyewe wa kutaka kuporomosha uongozi dhalimu katika mataifa mengi barani Afrika. Kwa upande mwingine, jina Shauri Yako linatokana na nomino mawaidha au nasaha au uamuzi wa mtu binafsi. Pia huweza kuwa kitenzi toa mawaidha, nasaha au maoni, pendekeza, eleza au ongoza. Hivyo, kundi la vijana wa Shauri Yako ni kundi



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ambalo linasheheni vijana, ambao wameamua kwa kauli moja kupigania uhuru wa bara la Afrika; kutoka kwenye uongozi dhalimu na wa kiimla wa viongozi Waafrika.

Mintarafu ya haya, mtafiti akiongozwa na lengo la kwanza la utafiti huu, alibaini kuwa kundi la Poromokeni, vijana wa Shauri Yako na Bewa la Pevu ni taashira za Waafrika wakombozi. Kwa mujibu wa Kimani Njogu katika tamthilia ya *Zilizala* (2006), bara la Afrika litapata uhuru kutokana na utu na ubinadamu wa Waafrika (uk. 80). Aidha anashikilia imani kuwa mataifa mengi ya Kiafrika yatajinasua kutoka kwenye meno ya ukoloni mamboleo, pale tu Waafrika watakaposhikamana, watakapoelekezana na watakapohimizana (uk. 80). Vijana barobaro ni taashira za Waafrika wakombozi barani Afrika.

**Kumba**

Kumba ni mmoja wa wahusika katika tamthilia ya *Zilizala*. Kitaashira, Kumba ni taashira ya jana ya Udenda. Udenda alitia juhudi kusahau jana yake kwa sababu hakupendezwa na historia yake. Hivyo, Udenda anaashiria viongozi Waafrika ambao hujisahaulisha jana yao. Wanapopanda ngazi ya kitabaka, husahau dhiki na matatizo wananchi wenzao wanayokumbana nayo kila uchao. Hili linawekwa bayana na Kumba anapomweleza Udenda kuwa yeye huona ajabu anapomuona Udenda akijitahidi kujisahaulisha utoto wake. Anamkumbusha kuwa jana yake haiwezi kumbanduka kwa vyovyote vile. Aidha amjuza kuwa jana yake Udenda ni kama mwenye tumbo na tumbole, havitengani. Kumba alimsisitizia Udenda kuwa yeye Kumba ndiye jana yake Udenda na hivyo, mradi Kumba yupo Udenda hatawahi kuitaliki jana yake (uk. 36).

**Memetuka na Puma**

Kimani Njogu amepatia mhusika uwezo wa kuumba wahusika. Mathalani, Mwalimu Sega ni mhusika aliyepewa uwezo wa kuumba wahusika katika mchezo wa Puma na Memetuka. Sifa za wahusika hawa wawili zinaingiliana hivi kwamba mhusika mmoja anajenga na kukamilisha sifa za mwenzake kwa njia moja au nyingine. Memetuka ni mhusika anayechezwa na mhusika Udenda katika mchezo huo. Ukweli ni kwamba mna mshabaha na ukuruba mkubwa sana kati ya Memetuka na Udenda. Hata hivyo, ilibainika kwamba ni wahusika ambao wanawakilisha taashira zisizo za kupendeza kwa jamii. Kiuyakinifu wanaweza kurejelewa kama adui wa maendeleo endelevu na maendeleo kwa jumla. Kwa upande mwingine, Puma ni mhusika aliyechezwa na Kumba katika mchezo huo. Vile vile ilibainika kuwa mna mshabaha mkubwa kati ya mhusika Puma na mhusika Kumba. Hakika wanakumbana na dhiki, dharau na usaliti si haba kutoka kwa rafiki zao.

Memetuka ni taashira ya viongozi wa Kiafrika. Viongozi ambao hupenda kuombwa na kuabudiwa na wananchi waliowachagua. Kwa upande mwingine, Puma ni taashira ya Waafrika katika mataifa masikini ya Afrika ambao huishia tu kupiga kura na kuwa watumwa wa viongozi wao. Ndiposa Puma anamuomba kwa unyenyekevu akiwa amepiga magoti na kusema kuwa: Nataka unisaidie Mheshimiwa Memetuka. Bila wewe Mheshimiwa siwezi chochote. Nakusihi! Waokoe watoto wangu! *(Memetuka anamtazama kwa dharau.)* (uk. 44).

Memetuka ni jina linalotokana na kung'ara au kutoa mwanga ghafla kama nuru ya radi inavyotokea. Hili ladhihirisha kuwa, mtu au kitu kinachorejelewa kama Memetuka ni taashira ya mja asiye na msimamo. Kwa mfano, Memetuka ni taashira ya viongozi Waafrika ambao hupepesuka katika uamuzi wao na hawana msimamo dhabiti. Mwanga wanaotoa wa uongozi huwa wa ghafla ili wananchi wasinufaike wala wasiweze kujiendeleza. Viongozi wengi Waafrika husheheni ubinafsi huu ambao huhakikisha kuwa mna dhiki



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

zinazotumiwa na wanasiasa kama ala za kujipigia upatu wakati wa kampeni. Kwa mfano, barabara mbovu, usalama uliodorora, upungufu au hata ukosefu wa hospitali na zahanati, janga la njaa na ukame, ukosefu wa ajira na elimu bora baina ya vijana.

Memetuka ni taashira ya mnyama nguruwe. Nguruwe ni mnyama mnene na mfupi afugwaye, mwenye pua kubwa na ndefu, miguu mifupi na mkia mfupi ambaye Waislamu hawali nyama yake kwa kuwa ni haramu. Nguruwe huhusishwa na uchafu, kukoroma, kukula sana, kukula chochote kinacholika bila kubagua, ulafi na unene. Hivyo, ni mnyama ambaye huashiria watu wenye ubinafsi, ulafi, woga, uzembe na wasiokuwa na mwelekeo kama Memetuka. Nguruwe ni taashira ya viongozi wengi barani Afrika, ambao ni wakorofi na wenye ubinafsi bila mithili.

Puma ni jina linalotokana na kupumua kwa kasi. Ni kuachilia pumzi kwa kasi kutoka kinywani; hema, tweta au kuwa na mchomo na maumivu makali sana, hasa katika uvimbe au jipu. Hivyo basi, Puma ni taashira ya Waafrika katika mataifa mengi ya Kiafrika ambao huishi wakihema kutokana na kukimbia dhiki, ufukara, maradhi, siasa mbaya, uongozi dhalimu na matatizo mengine mengi. Viongozi na waajiri kwa jumla huwadharau wananchi masikini na kuwatumia kama karatasi ya kuchambia. Memetuka alimdharau mfanyakazi wake Puma. Alidhihirisha hili kupitia mabadiliko aiyomfahamisha Puma kuwa, kuanzia siku ile ingebidi Puma kutuma mtu mara tu angetaka mshahara wake amchukulie. Memetuka alilalamika kuwa harufu ya Puma ilikirihisha na kumkera yeye kiwango kwamba ilimzuia kupumua vyema. Alilalama kuwa alishindwa hata kumega chakula baada ya Puma kumkaribia na kisha kuondoka (uk. 46). Hili laashiria jinsi viongozi barani Afrika wanavyochukizwa na harufu ya ufukara inayotokana na Waafrika wengi ambao ni maskini.

Kwa upande mwingine, Memetuka ni taashira ya viongozi wa Kiafrika. Wengi wao hujiona wa hadhi ya juu kuliko binadamu wengine. Hakika wao hujiona watu na kuwachukulia wananchi kama viumbe duni visivyofaa kuwakaribia wala kuhusishwa nao. Kwa mfano, Memetuka alimkumbusha Puma kuwa: Umesahau hadhi yangu katika jamii? watu wakiniona bandani watafikiri nini? Banda ni lako kulishughulikia (uk. 46). Ama kweli ni viongozi wa kusahau kuliko ngiri. Lile banda wasiotaka kuhusishwa nalo, ni taashira ya taifa linalowasheheni wao pia, lakini hawatambui kuwa wenyewe ndio wanaotoa ule uvundo unaowakirihi.

Puma ni taashira ya wananchi fukara Waafrika wanaogaragara katika bahari la ulofa ili kujinusuru bila mafanikio. Umaskini huu hupaliliwa na kunyunyiziwa maji na viongozi waliochaguliwa. Hili ladhihirishwa na Memetuka anayemkejeli Puma kuhusiana na suala la akaunti ya benki. Mshahara anaolipwa Puma hautoshi na hivyo umaskini umemvaa mithili ya suti ya Adamu. Mathalani, Puma anapoulizwa kwa nini hana akaunti ya benki, anajibu kuwa hana pesa za kuweka. Hii ni kwa sababu chochote alicholipwa kama mshahara hutumika hata kabla hakijapata joto la mfuko. Pesa kidogo alizolipwa Puma na Memetuka hazikutosha kukidhia hata mahitaji ya kimsingi. Puma alikiri kuwa kile kipato kiliingia na kutoka mfukoni kama kwamba kilifukuzwa kwa maonyo makali (uk. 46).

Kadhalika, Puma ni taashira ya mabadiliko. Puma anaashiria wananchi wazalendo katika mataifa fukara ya Afrika, ambao huchoshwa na ufidhuli na ukatili wa viongozi na hivyo kuwang'oa mamlakani. Memetuka alihisi woga kutokana na tisho lililodhihirisha dalili za mabadiliko. Kwa mara ya kwanza, Puma alimkosoa mwaajiri wake Memetuka bila woga. Jambo hili lilimfadhaisha Memetuka na kumpa kiwewe. Ndiposa



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

alimkemea Puma kwa kumwuliza kuwa: "Unamkosoa mwajiri wako? Tangu lini ukaacha kuwa yule Puma mtiifu niliyemwokota mapipani? *(Kwa ukali.)* Unanikosoa?" (uk. 48) Hili laashiria woga walionao viongozi Waafrika kuhusu mabadiliko. Ndiposa wengi hung'ang'ania na kukatalia kwenye mamlaka kama ndio uhai wao.

Memetuka ni taashira ya viongozi Waafrika wanaowanyanyasa na kuwanyang'anya wananchi wazalendo mali yao. Mazungumzo kati ya Memetuka na Puma yanasawiri taswira halisi, jinsi viongozi hunyakua hata vya walalahoi bila huruma. Kwa mujibu wa Puma Memetuka alinyakua shamba la marehemu mamake Puma; Mekati. Puma alinunua ardhi mbali na mji asije akanyang'anywa na Memetuka. Puma akiwa amesimama mjiko alimjuza Memetuka kuwa yeye ni ila si alikuwa mwanawe Jemadari Mekati. Jemadari Mekati alikuwa mpigania ukombozi wa nchi ya Rutuba. Memetuka ambaye ni taashira ya viongozi dhalimu wa barani Afrika alishangaa kusikia kuwa Mekati alikuwa mamake Puma. Hata hivyo, hajuti wala haoni haya kunyakua shamba la Jemadari aliyepigania ukombozi wa nchi yao. Memetuka ang'ang'nia kuwa mamake Puma Mekati alimuuzia shamba lake hata kabla ya Puma kuzaliwa. Alishikilia msimamo kuwa stakabadhi halali alikuwa nazo kupitia kijikaratasi alichotoa baada ya kuchakura mifukoni mwake kilichokuwa na sahihi ya Jemadari Mekati. Ukweli ni kuwa sahihi ilikuwa yake Jemadari Mekati lakini Memetuka hakumlipa hata senti ya fedha walizokuwa wameagana kama malipo ya shamba la Twaa ya Kusudi. Alimpunja Mekati shamba pasipo kuona haya wala huruma. Puma anabaki kulalamikia jiwe kuwa mamake hakulipwa chochote. Ilikuwa kesi ya mbuzi kuamuliwa na chatu (uk. 49).

Familia yake Puma huishi kwa dhiki na ulofa uso kifani. Puma hana nyumba yake mwenyewe wala shamba. Hata hivyo, alikuwa na ndoto ya kusomesha watoto wake na kununua shamba. Mamake Puma ni marehemu Jemadari Mekati, ambaye alikuwa mpigania ukombozi wa nchi ya Rutuba. Mamake Puma alikuwa na shamba kubwa, lakini Memetuka alilinyakua na kulifanya lake. Kutokana na kutolipwa shamba lake na Memetuka, mamake Puma alipatwa na ugonjwa wa moyo na akaaga dunia. Puma alikosa mlezi na ikambidi kuishi kwenye mapipa. Ilibainika kwamba familia yake Puma ilikuwa inahema kutokana na dhiki walizokumbana nazo.

Mabinti zake Puma ni taashira za mataifa maskini ya Kiafrika. Taifa ndilo husheheni wananchi na kuwapa mandhari mazuri ya kuishi. Hivyo basi, kitaashira, kuhatarisha maisha ya binti mmoja ni kuhatarisha maisha ya wananchi wa taifa nzima la Kiafrika. Puma kama mpiganiaji ukombozi na haki za wananchi anapigania mataifa fukara ya Afrika, kutoka kwenye minyororo ya Wazungu weusi kama Memetuka. Ndiposa anatetea haki za mabinti zake kwa ujasiri na kusema kuwa: "Nahitaji mshahara wangu. Ninawalipia mabinti zangu karo" (uk. 50). Hakika elimu ndiyo mojawapo ya silaha nzuri ya kupambana na ulofa, uongozi mbaya na changamoto chungu nzima zinazoyakumba mataifa mengi barani Afrika. Memetuka alibaini ukweli huu na ndio maana anakuwa kikwazo kikuu.

**Inspekta**

Inspekta ni taashira ya Waafrika wachache wazalendo. Msimamo wake wa uzalendo ni taashira ya matumaini kwa Waafrika wengi kuwa mna siku itafika na mambo yatatengea, wazalendo kama Inspekta wakiwa. Ni mhusika anayeashiria matumaini barani Afrika kuwa sio kila afisa wa serikali aliye na uvundo wa ufisadi. Anatia motisha wazalendo wengi wanaopigania uhuru wa Afrika na kuwapa moyo kuendelea na mapambano. Mathalani, anaposema kuwa: "*(Akisimama mjiko.)* Kwa mujibu wa sheria za nchi siruhusiwi kuchukua bahasha kama hizi. Ni kishawishi kibaya; na ni hatari" (uk. 54). Kitendo hiki



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | March. -2020|
Received: 18.02.2020; Accepted 20.02.2020; Published: 10.03.2020 at www.editoncpublishing.org
Antony Kago Waithiru et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kinawapa Waafrika wengi matumaini na imani kwa baadhi ya ofisi za serikali na katika katiba ya sheria ya nchi husika. Ni mwanga unaowapa wengi ujasiri wa kufanya kazi katika ofisi za kiserikali ili wawe maajenti wa mapinduzi na mabadiliko chanya. Kwa mfano, Inspekta anaposema kuwa: Sheria za nchi zanizuia. Siwezi kuchukua bahasha hiyo japo nahitaji (uk. 55). Kuashiria kuwa kunao wazalendo ambao wanaamini katika kufuata sheria, haki, ukweli na usawa.

**Hitimisho**

Matini hii imetathmini kipengele mojawavyo vya taashira katika tamthilia za baada ya 2000 za Kimani Njogu. Kipengele kilichoangaziwa ni kile cha taashira za wahusika. Tamthilia za baada ya 2000 zimetumia mbinu hii ya taashira kupatia lugha leseni kuwasilisha masuala yanayoweza kuibua hisia kali au hata kupasha ukweli wa mambo ukiwa uchi. Katika matini hii mwandishi ameweza kuficha kasumba kwa kutumia mbinu ya taashira kuwasilisha ujumbe alionuia kwa kutumia wahusika na majina yao kitaashira. Inabainika kuwa taashira ni mbinu inayotumiwa na wengi katika kuwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache yenye maana yenye uketo zaidi na kwa muda mchache. Ikizingatiwa kwamba katika kazi za kifasihi, ujumbe huwasilishwa kupitia wahusika wanaoumbwa na mwandishi wa kazi husika, Kimani Njogu ametumia mbinu ya taashira kufanikisha mawasiliano katika tamthilia ya *Zilizala*.

**MAREJELEO**

King'ora, M. N. (2014). "Utendaji Katika Tamthilia za *Sudana* na Kimya Kimya Kimya". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Njogu, K. (2006). *Zilizala*. Nairobi, Kenya: Longman Kenya Ltd.

Njogu, K. na Chimerah, R; (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

United Bible Societies (2004). *The Holy Bible*. Printed in China.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Pubishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publisher.



© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org